# NISHATI
HABARI ZA NISHATI

# News Bulletin

www.nishati. go.tz | Wizara ya Nishati | wizara_ya_nishati_tanzania | @Nishati2017 | Wizara ya Nishati

Toleo Namba 10 | *Limesambazwa kwa Taasisi na Idara zote* **NISHATI** | Januari 1-31, **2020**


# UJENZI MRADI WA UMEME RUSUMO WAZIDI KUSHIKA KASI

## WAFIKIA ASILIMIA 59



*Mawaziri wanaohusika na usimamizi wa Mradi wa umeme wa Rusumo (megawati 80), wakikagua maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya mradi huo Desemba 6, 2019. Kutoka kushoto ni Waziri wa Nishati na Migodi (Burundi) Mhandisi Come Manirakiza, Waziri wa Nishati (Tanzania) Dkt Medard Kalemani na Waziri wa Miundombinu (Rwanda) Balozi Claver Gatete.*



*Mwonekano wa miundombinu mbalimbali ya Mradi wa Umeme wa Rusumo. Taswira hizi zilichukuliwa wakati Mawaziri wanaohusika na usimamizi wa Mradi huo kutoka nchi husika za Tanzania, Burundi na Rwanda walipofanya ukaguzi wa maendeleo yake, Desemba 6, 2019.*

**WIZARA YA NISHATI TUNAWATAKIA WASOMAJI WETU NA WATANZANIA WOTE HERI YA MWAKA MPYA**

**2020**


**JARIDA HILI LINATOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**

**Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma**



*Waziri wa Nishati (Tanzania) Dkt Medard Kalemani, akiongoza kikao cha majumuisho na utoaji taarifa kwa waandishi wa habari, kuhusiana na Mkutano wa 11 wa Mawaziri wanaosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo kutoka nchi husika ambazo ni Tanzania, Rwanda na Burundi. Mkutano huo ulifanyika Desemba 6, 2019 Ngara.*

# UJENZI MRADI WA UMEME RUSUMO WAFIKIA ASILIMIA 59

***VERONICA SIMBA – NGARA***

Mradi wa ujenzi wa kufua umeme wa maji (megawati 80) wa Rusumo, unaotekelezwa kwa ushirikiano wa nchi za Tanzania, Burundi na Rwanda, umefikia asilimia 59 kutoka 32 iliyokuwa imefikiwa Juni mwaka huu.

Hayo yamebainishwa na Mwenyekiti (aliyemaliza muda wake) wa Mawaziri wanaohusika na Mradi huo kutoka nchi husika, ambaye ni Waziri wa Nishati (Tanzania), Dkt Medard Kalemani, wakati akitoa mrejesho wa mkutano wa 11 wa Mawaziri hao kwa waandishi wa habari, uliofanyika Desemba 6, 2019 wilayani Ngara, mkoani Kagera.

Waziri Kalemani alisema kuwa baada ya kufanya ukaguzi, yeyé na mawaziri wenzake wameridhishwa na maendeleo ya mradi husika, lakini wametoa maelekezo kadhaa kwa mkandarasi na timu ya wataalamu wanaosimamia mradi huo, ili kuhakikisha unakamilika kwa wakati na viwango stahiki kama ilivyokusudiwa.

"Tumeona kuna hali nzuri ya utekelezaji. Hata hivyo, tumetaka mkandarasi pamoja na wasimamizi wakamilishe kazi ndani ya muda uliopangwa ambao ni Februari, 2020."

Katika hatua nyingine, mawaziri hao wamekataa ombi la mkandarasi kuongezewa muda wa kukamilisha mradi huo ambapo aliomba akabidhi mradi Julai 2021 badala ya Februari mwakani.

Akielezea sababu za mkandarasi kuomba kuongezewa muda, Waziri Kalemani alisema ni kutokana na malalamiko ya baadhi ya wananchi wanaoishi jirani na eneo unapotekelezwa mradi, ambao waliwasilisha malalamiko ya nyumba zao kuathiriwa na milipuko inayofanyika.

"Kwa sababu hiyo, mkandarasi ameomba muda zaidi ili afanye tathmini kuhusu malalamiko hayo na ajipange kufanya milipuko isiyo na madhara kwa jamii. Hata hivyo, sisi tumekataa ombi lake na kumtaka akamilishe kazi ndani ya muda uliopangwa."

Akifafanua zaidi, Waziri alieleza kuwa, yeyé na mawaziri wenzake, wamemtaka mkandarasi kuwasilisha mapendekezo yanayoeleza bayana kwanini aongezewe muda ili wajiridhishe maana wao wanaamini kwa kutumia utaalamu wake, mkandarasi anaweza kutekeleza mradi huo kwa wakati huku akizingatia kufanya milipuko isiyo na madhara kwa wananchi.

Akizungumzia suala la uwepo wataalamu wanaosimamia mradi husika, Dkt Kalemani alisema kuwa wameagiza ifikapo mwisho wa mwezi huu, timu ya wataalamu hao 12 wakiwemo wapya waliopatikana hivi karibuni; wahakikishe wanahamia kwenye nyumba zao zilizoko eneo la mradi ambazo mawaziri hao wamejiridhisha kuwa zimekamilika, baada ya kuzikagua.

Mawaziri husika wamewataka wasimamizi hao wa mradi kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao ipasavyo kwa weledi na uaminifu ili ukamilike kwa wakati na viwango vinavyotakiwa.

Vilevile, wameagiza mradi huo unaogharimu Dola za Marekani milioni 340 utekelezwe kwa mtindo wa kazi zote husika kwenda sambamba.

Waziri Kalemani alizitaja kazi hizo kuwa ni pamoja na ujenzi wa mtambo wa uzalishaji, ujenzi wa bwawa, ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kutoka eneo la mradi kupitia Nyakanazi (Tanzania) umbali wa kilomita 94, Rwanda (kilomita 161) na kutoka Rusumo hadi Burundi (kilomita 194).

Awali, Waziri Kalemani alilazimika kusimama na kuzungumza na wananchi wa Rusumo ambao walikuwa na malalamiko ya kudai fidia ambapo aliagiza fidia zao zianze kulipwa mara moja kuanzia Desemba 15, mwaka huu.

Aidha, aliagiza wananchi hao waletewe matenki ya kuhifadhia maji safi ili waondokane na adha ya kutumia maji yasiyo salama kutoka Mto Rusumo, ambayo walikuwa wakikabiliana nayo.

Katika Mkutano huo wa 11 wa Mawaziri husika, Mwenyekiti anayemaliza muda wake, Dkt Medard Kalemani (Tanzania) alikabidhi nafasi hiyo kwa Mwenyekiti mpya ambaye ni Waziri wa Nishati na Migodi kutoka Burundi, Mhandisi Come Manirakiza.





# BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**

**Dkt. Hamisi Mwinyimvua**
(Katibu Mkuu
Wizara ya Nishati)

**Mhariri**

**Veronica Simba**
(Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini)

**Waandishi**

**Veronica Simba**
**Teresia Mhagama**
**Zuena Msuya**
**Hafsa Omar**

**Msanifu Kurasa**

**Lucas Gordon**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi: +255-26-2320148 au

Fika Ofisi ya Mawasiliano Mtumba Dodoma, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma

*www.nishati. go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*


# MAONI/KATUNI

## HIMA WANANCHI, TUCHANGAMKIE MIRADI YA UMEME KATIKA MAENEO YETU

Sote tunatambua kazi inayoendelea ya usambazaji umeme vijijini kupitia mradi wa usambazaji umeme vijijini ambao umefikia Awamu ya Tatu, mzunguko wa kwanza (REA III) na vijiji zaidi ya 8000 vimesambaziwa umeme kupitia mradi wa umeme vijijini wa Awamu ya Kwanza, Pili na Tatu mzunguko wa kwanza.

Ili miradi hiyo ya umeme vijijini ilete matokeo chanya, Serikali iliamua kuwa wananchi wote vijijini waunganishe umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 tu.

Katika baadhi ya maeneo na vijiji tumeshuhudia wananchi wengi wakichangamkia fursa hiyo na kuunganisha umeme kwa wingi mara mradi unapofika kijijini lakini kuna baadhi ya maeneo pia wananchi wameonekana kusuasua kuunganisha umeme licha ya umeme kufika kwenye maeneo yao.

Hivi karibuni, akiwa katika kijiji cha Chemkeni, kata ya Igwisi, Wilaya ya Kaliua, Mkoani Tabora, Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani, alikagua nyumba ambazo hazijaunganishwa umeme kijijini humo na kusikitishwa na uunganishaji hafifu wa umeme.

Kutokana na hilo, alisema kuwa Serikali itaanza kuchua hatua kwa wananchi wote ambao hawataunganisha umeme kwenye nyumba zao, ambao wana uwezo wa kulipia shilingi 27,000/= kwa kuwa Serikali inatumia fedha nyingi kupeleka umeme kwenye maeneo hayo ili ulete tija na hatimaye kukuza uchumi wa nchi.


Akitolea mfano, alisema kuwa, kwa Mkoa wa Tabora, Serikali imetenga shilingi Bilioni 36 ili kusambaza umeme vijijini kupitia mradi wa REA III, mzunguko wa kwanza hivyo kuna umuhimu wa wananchi kutambua juhudi hizo za Serikali kwa kuunganisha umeme kwa wingi ambao utawasaidia kwenye shughuli za kijamii na kiuchumi.

Akiwa wilayani Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu pia alisisitiza kuhusu suala la kuunganisha umeme kwa wananchi na kuitaka TANESCO kuangalia namna bora ya kuwawezesha wateja kulipia gharama za umeme katika majumba yao, ikiwezekana kuwakopesha na baadaye walipie kupitia LUKU au Ankara zao au kuwawekea utaratibu wa kulipia kidogo kidogo ili kila mmoja aweze kuunganishwa na umeme.

Aidha, aliwaelekeza TANESCO kutokataa fedha pale mteja anapotaka kulipa kwa awamu, isipokuwa waweke utaratibu mzuri wa malipo hayo kwa lengo la kumsadia mteja yule ambaye hawezi kuzilipa zote kwa mara moja ili aunganishiwe umeme.

Kutokana na juhudi hizi zinazofanywa na Serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wake vijijini na mijini wanapata huduma ya umeme, ndio mana tunasema kuwa ni muhimu kwa wananchi pia kutambua jitihada hizi za Serikali kwa kuichangamkia miradi hii ya umeme mara inapofika katika maeneo yao.

## Katunika Ki-nishati



# MATUKIO PICHANI






*Waziri wa Nishati (Tanzania) Dkt Medard Kalemani, akiongoza Mkutano wa 11 wa Mawaziri wanaosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo kutoka nchi husika ambazo ni Tanzania, Rwanda na Burundi (hawapo pichani). Mkutano huo ulifanyika Desemba 6, 2019 Ngara.*



*Waziri wa Nishati (Tanzania – wa pili kutoka kushoto) Dkt Medard Kalemani na mawaziri wenzake kutoka Rwanda (Balozi Claver Gatete – wa tatu kutoka kushoto) na Burundi (Mhandisi Come Manirakiza - kushoto), wakikagua na kusikiliza maelezo kuhusu hatua iliyofikiwa katika kutekeleza ujenzi wa mradi huo, Desemba 6, 2019.*



*Waziri wa Nishati (Tanzania) Dkt Medard Kalemani na mawaziri wenzake kutoka Rwanda (Balozi Claver Gatete) na Burundi (Mhandisi Come Manirakiza), wakikagua na kusikiliza maelezo kuhusu hatua iliyofikiwa katika kutekeleza ujenzi wa mradi huo, Desemba 6, 2019.*



*Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo, Mhandisi Innocent Luoga (katikati), akifuatilia hoja zilizokuwa zikijadiliwa katika Mkutano wa 11 wa Mawaziri wanaosimamia Mradi husika kutoka nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi (hawapo pichani), Desemba 6, 2019.*



*Mjumbe wa Kamati ya Ufundi ya Kampuni inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo, Mhandisi Salum Inegeja (kulia) akimfafanulia jambo kuhusu mradi huo Katibu wa Waziri wa Nishati, Mhandisi Robert Dulle (kushoto), wakati Mawaziri wanaohusika na usimamizi wa Mradi kutoka nchi husika za Tanzania, Burundi na Rwanda, walipofanya ukaguzi wa maendeleo yake, Desemba 6, 2019.*







*Mwonekano wa miundombinu mbalimbali ya Mradi wa Umeme wa Rusumo. Taswira hizi zilichukuliwa wakati Mawaziri wanaohusika na usimamizi wa Mradi huo kutoka nchi husika za Tanzania, Burundi na Rwanda walipofanya ukaguzi wa maendeleo yake, Desemba 6, 2019.*

NA ZUENA MSUYA,
PWANI

# Mgalu aonya vitendo vya rushwa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, amepiga marufu tabia ya baadhi ya watu kutoa au kupokea rushwa ili waweze kupata ajira na fursa mbalimbali ikiwepo biashara katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere utakaozalisha umeme wa kiasi cha megawati 2115.

Aliyasema hayo, Desemba 13, 2019 alipofanya ziara ya kikazi katika Kjiji cha Mloka wilayani Rufiji mkoani Pwani kwa lengo la kusikiliza malalamiko ya baadhi ya wakazi wa eneo hilo juu ya utaratibu unaotumika katika kuwapatia watu ajira katika mradi huo ambapo pia aliwasha umeme katika kijiji cha Kipo wilayani humo.

Alisema kuwa, Serikali haitaki kusikia tuhuma za kuomba rushwa,upendeleo, simu zinazolelekeza mtu kupewa ajira pamoja na urasimu,vilevile kuwataka wahusika wafuate utaratibu mzuri kulingana kada zinazotakiwa kwa uwiano sahihi kwakuwa mradi huo unatekelezwa kwa unatumia kodi za watanzania wote.

Aidha aliweka wazi kuwa, mradi huo ni mkubwa kutekelezwa nchini, ambapo Rais Dkt. John Magufuli aliwaahidi watanzania na kuweka malengo kuwa mradi huo utatoa ajira na fursa mbalimbali, hivyo wao kama viongozi wanapaswa kusimamia hilo ili kuwatendea haki watanzania waweze kunufaika na ujenzi wa mradi husika na kujiongezea kipato.

Aliwataka wale wote waliopewa dhamana ya kusimamia upatikanaji wa ajira ama fursa za shughuli mbalimbali katika mradi huo, kutumia busara na kufuata utaratibu, pia wasidhani kuwa mradi huo ni wa kwao kwa kufanya kile wanachokiona na kupenda wao.

"Watafutaji wa ajira, vibarua maarufu kama "Wasoteaji" ni marufuku kutoa fedha ili mpate ajira, kama utatumia fedha hizo kuweka mtego kuwakamata wahusika wanaopokea na kutoa rushwa hilo tutakuunga mkono na endapo tutamkamata utapata ajira kwa sababu umetusaidia, hatutaki mradi huu uwe na kasoro ya rushwa na ni marufuku." alisisitiza Mgalu.

Baada ya kusikia malalamiko na changamoto hizo aliahidi kwenda kuzifanyia kazi kwa kufanya mashauriano na kujadili na sekta nyingine ili kupata namna bora ya kuwawezesha vijana kufanya kazi na akina mama kupata fursa ya kufanya biashara ndogondogo ikiwemo kuuza vyakula.



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akionyesha moja ya karatasi za matangazo katika ubao wakati akizungumza na vijana na kina mama kutoka Mikoa mbalimbali nchini walioweka kambi katika Ofisi ya Kijiji cha Mloka wilayani Rufiji mkoani Pwani, wakisubiri kupata ajira pamoja na fursa za biashara katika ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere.*

Akiwa katika ziara hiyo, Mgalu alishuhudia malori yaliyobeba saruji yakiwa yamesimama huku yakiwa na mizigo, ambapo alielezwa kuwa malori hayo yamezuiwa kuingia ndani ya eneo la mradi kushusha mzigo wa zaidi ya siku Tano kutokana na kukosa kibali cha kuwaruhusu kuingia ndani.

Kutokana na maelezo hayo, alitoa onyo kuwa yeyote atakayeweka vikwazo ama urasimu katika kuingiza vifaa katika mradi huo kuwa atachukuliwa hatua za kisheria na kinidhamu kwa kuwa wanaofanya hivyo hawana nia njema na mradi huo bali wana nia ya kukwamisha ama kuchelewesha mradi huo.

"Nimesikitika sana kuona malori ya saruji hapa nje eti yanakaa hapa kwa zaidi ya siku Tano kusubiri kibali, kibali gani hicho, anayezuia kutoa hicho kibali ni nani, nataka kumfahamu,na kwa nini azuie wakati saruji inahitajika huko ndani? hatutakubali kukwamishwa na chochote, na anayetaka kutukwamisha atakwama yeye na ikibainika atachukuliwa hatua." alisema Mgalu.

Alisisitiza kuwa, tayari ilishaundwa kamati maalum kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali inayofanya kazi ya kusimamia na kurahisisha mwenendo mzima wa ujenzi wa mradi huo, kwa kuweka malengo na mikakati mbalimbali ikiwepo utoaji wa vibali kwa wakati na visichukue zaidi ya siku Tatu ikiwa ni pamoja na vile vibali vya ukaazi kwa wakandarasi wageni.


Hata hivyo baadhi ya vijana na wakazi wa eneo hilo wameomba Serikali itumie utaratibu mzuri wa kuwapatia ajira ili wasiweze kukaa eneo hilo muda mrefu hali ya kuwa wameshawasilisha taarifa zao sehemu husika na wengine wamefanya majaribio wanasubiri majibu.

Katika hatua nyingine Naibu Waziri, aliwasha umeme katika kijiji cha Kipo wilayani Rufiji, pamoja na kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu (REA III), kazi inayoendelea katika mikoa mbalimbali nchini.

Aliendelea kuwasisitiza REA na TANESCO kuwa wasiruke kijiji kwa kuwa utekelezaji wa REA III mzunguko wa pili unaoanza Januari 2020 ni wa mwisho katika kusambaza umeme vijijini, miradi itakayofuata ni kwa ajili ya Vitongoji.



*Baadhi ya vijana na akimama kutoka Mikoa mbalimbali nchini walioweka kambi katika Ofisi ya Kijiji cha Mloka wilayani Rufiji mkoani Pwani, wakinyoosha mikono juu kuunga mkono maagizo ya Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alipofika katika kijiji cha Mloka kusikiliza malalamiko yao ya ajira pamoja na fursa za biashara katika ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere.*



*Baadhi ya Mabegi ya vijana na akina mama kutoka mikoa mbalimbali waliloweka kambi katika Ofisi ya Kijiji cha Mloka wilayani Rufiji mkoani Pwani, wakisubiri kupata ajira pamoja na fursa za biashara katika ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, yakiwa yamehifadhiwa nje ya varanda ya moja ya nyumba za wakazi wa kijiji hicho.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu ( katikati) akizungumza na vijana na akimama kutoka Mikoa mbalimbali nchini walioweka kambi katika Ofisi ya Kijiji cha Mloka wilayani Rufiji mkoani Pwani, wakisubiri kupata ajira pamoja na fursa za biashara katika ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere.*



*Mmoja wa akina Mama (kushoto) akimueleza Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, ambavyo waliahidiwa kupata fursa za biashara na kuishi zaidi ya miezi miwili katika kijiji cha Mloka akisubiri fursa hiyo, mama huyo anatokea mkoani Dar Es Salaam.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akizungumza na wakazi wa kijiji cha Kipo wilayani Rufiji mkoani Pwani wakati alipofika kuwasha umeme.*



*Mzee Amir Mponda (katikati) akizungumza na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (hayupo pichani) kuhusu suala la ajira na fursa za biashara katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere .*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (watatu kushoto waliosimama) akiwa katika picha ya pamoja viongozi wa serikali za mitaa na baadhi ya akimama wa kikundi cha wenye Ulemavu, baada ya kuwapa msaada wa majora ya vitambaa vya kushona sare za shule, katika Kijiji cha Ikwiri Kati wilayani Rufiji mkoani Pwani.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (pili kulia) akikata utepe katika moja ya duka la kuuza dawa za Binadamu kuashiria kuwasha umeme katika kijiji cha Kipo, wilayani Rufiji mkoani Pwani.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. Hamisi Mwinyimvua (katikati), Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi (wa Tatu kutoka kulia) na Kamishna Msaidizi wa Gesi, Sebastian Shana (wa kwanza kulia) wakiwa na watendaji wa kampuni ya GASCO na wataalam kutoka Wizara ya Nishati katika mitambo ya Gesi ya Madimba mkoani Mtwara.*

# KATIBU MKUU NISHATI AKAGUA MITAMBO YA GESI SONGONGO NA MNAZI BAY

Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Dkt. Hamisi Mwinyimvua, amefanya ziara ya kikazi katika mitambo ya kuzalisha, kuchakata na kusafirisha gesi asilia iliyopo kisiwani Songo Songo mkoani Lindi, na ile ya Madimba na Mnazi Bay Mkoani Mtwara kwa lengo la kukagua maendeleo ya uzalishaji na uchakataji wa Gesi Asilia katika maeneo hayo.

Ziara hiyo aliifanya tarehe 11 Disemba, 2019 akiwa ameambatana na Kamishna wa Gesi na Petroli, Adam Zuberi, Kamishna Msaidizi wa Gesi, Sebastian Shana na watendaji kutoka kampuni tanzu ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ya GASCO inayoshughulikia masuala ya Usambazaji Gesi .

Pamoja na ukaguzi wa maendeleo ya uzalishaji na uchakataji wa Gesi Asilia katika maeneo hayo, ziara hiyo ililenga kubaini kama kuna changamoto ambazo zinaweza kukwamisha upatikanaji wa Gesi Asilia nchini.

Baada ya ukaguzi wa mitambo hiyo, Katibu Mkuu aliwapongeza watendaji wa TPDC na GASCO kwa jinsi walivyoweza kujenga uwezo kwa maafisa wake ambao ndio wanaendesha mitambo hiyo ya kuchakata Gesi Asilia bila kutegemea wataalam kutoka nje ya nchi.

Vile vile, aliwagiza wataalam hao kusimamia vizuri mitambo hiyo ili kuimarisha hali ya upatikanaji wa Gesi Asilia ambayo inatumika kwa matumizi mbalimbali nchini ikiwemo kuzalisha umeme, kutumika majumbani, viwandani na kwenye magari.



*Mtaalam anayefanya kazi katika mitambo ya kuchakata Gesi Asilia ya Madimba mkoani Mtwara akitoa maelezo kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt Hamisi Mwinyimvua (wa Pili kushoto) na wataalam wengine kuhusu kazi zinazofanywa kwenye kituo hicho.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. Hamisi Mwinyimvua (wa Tatu kulia), Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi (wa Pili kulia) na Kamishna Msaidizi wa Gesi, Sebastian Shana (wa Tano kutoka kushoto) wakiwa na watendaji wa kampuni ya GASCO na wataalam kutoka Wizara ya Nishati katika mitambo ya Gesi ya Songosongo mkoani Lindi.*

# Mgalu aliridhishwa na miundombinu ya umeme mradi wa SGR



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (mwenye kilemba) akiangalia kazi ya ujenzi wa mmoja wa misingi ya kusimika nguzo kubwa za umeme za kV 220 zitakazotumika katika reli ya kisasa, inayoendelea katika njia ya kusafirisha umeme.*



*Mafundi wakiendela na kazi ya kumwaga zege chini ardhini ikiwa ni ujenzi wa msingi wa nguzo ya kusafirisha umeme mkubwa utakaotumika katika reli ya kisasa.*



*Muonekano wa moja ya nguzo kubwa itakayosafirisha umeme wa kV 220 katika reli ya kisasa baada ya kusimamishwa tayari kwa kupitisha nyaya.*

***NA ZUENA MSUYA, DAR ES SALAAM***

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu amesema ameridhishwa na ujenzi wa miundombinu ya njia ya kusafirisha umeme wa kV 220 inayoendelea kujengwa katika Reli ya kisasa kutoka jijini Dar es salaam hadi mkoani Morogoro .

Mgalu alieleza hayo Desemba 7, 2019 baada ya kufanya ziara ya kukagua maendeleo ujenzi wa miundombinu hiyo kuanzia Kituo cha Kinyerezi, Pugu hadi Kisarawe jijini Dar es salaam ambapo asilimia 70 ya kazi hiyo imekamilika.

Alitumia ziara hiyo kuwathibitishia watanzania kuwa mradi huo wa ujenzi wa njia ya umeme utakamilika kwa wakati kulingana makubaliano ya mkataba na umeme upo mwingi na wa kutosha kuwezesha reli hiyo kufanya kazi yake wakati wote.

Alifafanua kuwa, ujenzi wa miundombinu ya njia ya kusafirisha umeme inatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2020 ili kutoa fursa ya kuanza majaribio ya safari kwa kutumia Treni ya umeme, kabla ya kuanza rasmi kwa safari hizo mwezi Julai, 2020.

"Niwatoe hofu wale wote wenye mashaka na usafiri wa reli kwa kutumia umeme, umeme upo mwingi na wa kutosha nchini, kwa sasa tunazalisha zaidi ya megawati 1,601, tunazotumia ni megawati 1,116 tu, pia kazi ya kujenga miradi mikubwa ya kuzalisha umeme mwingi zaidi inaendelea, ukiwemo Mradi wa Julius Nyerere katika bonde la mto Rufiji, Rusumo na Kinyerezi." alisisitiza Mgalu.

Pia alikagua ghala za kuhifadhia vifaa mbalimbali vinavyotumika katika ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme lililopo Kibaha mkoani Pwani na kushuhudia uwepo wa vifaa vya kutosha kukamilisha ujenzi wa njia hiyo.

Aidha aliwataka wasimamizi wa mradi huo kuwalipa vizuri wafanyakazi /vibarua wanaofanya kazi katika mradi huo ili na wao wafurahie na kunufaika kuwepo kwa mradi huo, vilevile aliwataka vibarua hao kufanya kazi kwa bidii, kuwa walinzi wa vifaa hivyo na miundombinu na kuweka mbele maslahi ya taifa.

Aidha, alilipongeza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kazi nzuri ya kusimamia utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya njia ya kusafirisha umeme mkubwa katika reli ya kisasa, na kuwataka kuongeza kasi zaidi ya ujenzi huo ili ikiwezekana ujenzi huo ukamilike kabla ya muda waliopewa.

Kwa upande wake, Msimamizi wa mradi huo kutoka TANESCO, Mhandisi Deogratius Msaki alisema kuwa kazi hiyo inaendelea vizuri licha ya changamoto ya kijiografia katika baadhi ya maeneo.

Aliweka wazi kuwa, mpaka sasa tayari wamesimamisha nguzo zaidi 120 kati ya 456 zitakazotumika kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, pia kazi ya kuweka vikombe na kuanza kuvuta nyaya imekwishaanza katika maeneo ambayo tayari usimikwaji wa nguzo umekamilika huku kazi hiyo ikiendelea na matarajio yao ni kuukabidhi mradi huo tarehe 28 Februari 2020.

# MATUKIO PICHANI



*Mafundi wakiendelea na kazi ya kusuka nondo kabla ya kumwaga zege, katika ujenzi wa msingi wa nguzo kubwa ya kusafirisha umeme wa kV 220, utakaotumika katika reli ya kisasa.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akitoa maelekezo kwa wasimamizi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme mkubwa utakaotumika katika reli ya kisasa baada ya kutembelea na kukagua ghala la kuhifadhia vifaa hivyo lililopo Kibaha, mkoani Pwani.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akizungumza na baadhi ya wafanyakazi/vibarua katika ghala la kuhifadhi vifaa vya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme mkubwa utakaotumika katika reli ya kisasa, lililopo Kibaha, mkoani Pwani.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akikagua baadhi ya vifaa vinavyotumika katika ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme mkubwa, katika mradi wa reli ya kisasa katika ghala la kuhifadhia vifaa hivyo lililopo Kibaha, mkoani Pwani.*



*Baadhi ya vifaa vinavyotumika katika ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme mkubwa utakaotumika katika reli ya kisasa vilivyohifadhiwa katika ghala lililopo Kibaha mkoani Pwani.*

# TUNA VIFAA VYA UMEME VINGI KULIKO MAHITAJI – DKT KALEMANI



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akizungumza na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Namtumbo, mkoani Ruvuma kueleza dhamira ya ziara yake wilayani humo, Desemba 10, 2019. Wa kwanza kulia ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Sophia Kizigo na kushoto kwa Waziri ni Mbunge wa Namtumbo, Mhandisi Edwin Ngonyani.*

**VERONICA SIMBA – NAMTUMBO**

Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani amewataka Mameneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) katika mikoa yote, kutowaambia wananchi kuwa kuna uhaba wa vifaa vya kuunganishia umeme kwani vilivyopo idadi yake ni kubwa kuliko matumizi ya nchi.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Namtumbo, mkoani Ruvuma, akiwa katika ziara ya kazi Desemba 10, 2019.

Akifafanua, Dkt Kalemani alisema baadhi ya watendaji wa shirika hilo hawatoi huduma ipasavyo kwa wateja, wakitumia kisingizio kuwa hawana vifaa husika zikiwemo nguzo, nyaya, transfoma na mita za luku, suala ambalo siyo kweli.

"Meneja yeyote atakayeshindwa kumuunganishia mwananchi umeme kwa kisingizio cha ukosefu wa vifaa, hatutamwelewa," alisisitiza Waziri.

Akitoa takwimu ya vifaa husika, Waziri alisema kwa sasa, nchi ina viwanda tisa ambavyo vinazalisha nguzo zaidi ya milioni mbili kwa mwaka wakati mahitaji ni milioni 1.2.

Vilevile, alisema mahitaji ya transfoma kwa nchi ni chini ya 210,000 wakati zinazozalishwa ni zaidi ya idadi hiyo kwa mwaka na kwamba nchi ina viwanda zaidi ya vinne vya kuzalisha transfoma.

Kwa upande wa mita za luku, alisema vipo viwanda vitatu vikubwa vinavyozalisha mita zaidi ya milioni mbili wakati mahitaji ni 1,490,000 kwa mwaka.

"Awali, tulikuwa na changamoto ya nyaya maana kulikuwa na kiwanda kimoja tu. Sasa hivi tuna viwanda vitano vinavyozalisha zaidi ya kilomita laki tano wakati mahitaji yetu ni chini ya laki 2.5 kwa mwaka.

Katika hatua nyingine, Waziri alisema hali ya upatikanaji umeme kwa mkoa wa Ruvuma ni nzuri na kwamba zipo changamoto chache ambazo serikali inazifanyia kazi.

Alisema, moja ya mikakati mikubwa inayotekelezwa ni kuunganisha kwenye gridi ya Taifa baadhi ya vijiji vya Namtumbo hadi Tunduru vilivyokuwa havijaungwa ili viwe na umeme wa uhakika.

Waziri aliieleza Kamati ya Ulinzi na Usalama kuwa, kazi hiyo inatarajiwa kukamilika Desemba 12 na kwamba ifikapo Desemba 13, 2019, gridi ya Taifa kutoka Songea – Namtumbo – Tunduru itawashwa na kuzima mashine inayotumia mafuta mazito iliyopo Tunduru.

Katika ziara hiyo, Waziri aliwasha umeme katika kijiji cha Mwangaza wilayani humo ambapo aliwasisitiza watendaji wa TANESCO kuwahamasisha wananchi wengi wajitokeze kulipia shilingi elfu 27 ili waunganishiwe umeme.

Alifuatana na viongozi mbalimbali akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Sophia Kizigo na Mbunge wa jimbo hilo Mhandisi Edwin Ngonyani. Viongozi hao kwa nyakati tofauti, waliipongeza Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa namna inavyopambana kuhakikisha wananchi wa vijijini wanafikiwa na huduma ya umeme.



*Sehemu ya umati wa wananchi wa kijiji cha Mwangaza, wilayani Namtumbo, Mkoa wa Ruvuma, wakishangilia kufuatia maelezo ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), kuhusu mikakati ya serikali kufikisha umeme kwa kila kaya. Waziri aliwasha rasmi umeme kijijini hapo, Desemba 10, 2019 akiwa katika ziara ya kazi.*

# Tanzania na Namibia wajadiliana kuhusu SACREEE

**NA ZUENA MSUYA, DODOMA,**

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu na Naibu Waziri wa Nishati wa Namibia, Kornelia Shilunga pamoja na ujumbe wake, wamekutana na kujadili kwa pamoja kuhusu Kituo cha Nishati Jadidifu na Matumizi bora ya Nishati cha nchi zilizo Kusini mwa Afrika (SACREEE).

Mgalu alikutana na ujumbe huo, Desemba 2, 2019, katika Ofisi za Wizara zilizopo jijini Dodoma, kwa lengo la kujadili suala la Tanzania kuweka saini katika mkataba wa makubaliano ya pamoja yaliyofikiwa na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) juu ya kuanzishwa kwa SACREEE.

Katika mazungumzo hayo, Mgalu aliueleza ujumbe huo kuwa, mpaka sasa Tanzania bado haijasaini Mkataba wa Makubaliano ya pamoja ya utekelezaji wa kituo hicho hadi pale uamuzi wa kuanzishwa kwa kituo hicho utakapoidhinishwa na Marais wa nchi wanachama wa SADC.

Aidha, Mgalu alisema baada ya kukamilika kwa taratibu za kisheria juu ya uanzishwaji wa SACREEE, Tanzania iko tayari kusaini mkataba kwa ajili kuwezesha kituo hicho ambacho Makao yake Makuu yako nchini Namibia.

Halikadhalika, Mgalu alisema kuwa Tanzania na Namibia ni nchi wanachama SADC hivyo ni dhahiri kwamba nchi hizo zitakuwa zikishirikiana kwa namna moja ama nyingine katika masuala mengine mbalimbali kupitia umoja huo.

Sambamba na hilo, alisema nchi hizo pia zinaweza kushirikiana kwa kuuziana umeme kupitia njia ya kusafirisha umeme wa kV400 inayojengwa kwa ajili ya kuunganisha gridi za Tanzania na Zambia kwa kuwa nchi hizo ni wanachama wa Mtandao wa Southern Africa Power Pool (SAPP) ambao uko chini ya SADC.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Namibia, Shilunga aliishauri Tanzania isaini mkatba huo ili SARCEEE isonge mbele kwa manufaa nchi wanachama pia alisema Namibia inaendelea kuhamasisha nchi zilizobaki zisaini mkataba huo.

Tayari nchi 8 kati ya 16 zimekwishakusaini Mkataba wa makubaliano ya pamoja ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya kuanzishwa kwa SACREEE ambayo ilizinduliwa mjini Windhoek nchini Namibia, Oktoba, 2018 na kuhudhuriwa na Mawaziri kutoka nchi wanachama wa SADC na Wakuu wa Taasisi za Kimataifa na Kikanda zinazohusika na sekta ya nishati.



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (kushoto) akiongoza majadiliano ya pamoja na Ujumbe kutoka Namibia,(kushoto) na Watendaji wakuu wa Wizara ya Nishati (kulia) kuhusu Kituo cha Nishati Jadidifu na Matumizi Bora ya Nishati cha nchi zilizo Kusini mwa Afrika (SACREEE) katika Ofisi ya Wizara ya Nishati Dodoma.*



*Watendaji Wakuu wa Wizara ya Nishati wakiwa katika majadiliano ya pamoja ya Kituo cha Nishati Jadidifu na Matumizi Bora ya Nishati cha nchi zilizo Kusini mwa Afrika (SACREEE) katika Ofisi ya Wizara ya Nishati Dodoma.*



*Naibu Waziri wa Nishati wa Namibia, Kornelia Shilungwa,( kulia) akiwa na ujumbe alioambatana nao wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, (hayupo pichani) wakati wa majadiliano ya pamoja kuhusu Kituo cha Nishati Jadidifu na Matumizi Bora ya Nishati cha nchi zilizo Kusini mwa Afrika (SACREEE) katika Ofisi ya Wizara ya Nishati Dodoma.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (kulia) na Naibu Waziri wa Nishati wa Namibia, Kornelia Shilunga( kushoto) waliokaa, wakiwa katika picha ya pamoja na ujumbe kutoka Namibia na Watendaji wakuu wa Wizara ya Nishati baada ya majadiliano ya pamoja kuhusu Kituo cha Nishati Jadidifu na Matumizi Bora ya Nishati cha nchi zilizo Kusini mwa Afrika (SACREEE) katika Ofisi ya Wizara ya Nishati Dodoma.*

# DKT KALEMANI AZINDUA KITUO CHA KUPOKEA NA KUTAWANYA NJIA KUU ZA UMEME -SIMIYU

**HAFSA OMAR -SIMIYU**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, amezindua Kituo cha Kupokea na Kutawanya Njia Kuu za Umeme (Switching Station) kilichopo katika kijiji cha Ng'ami, eneo la Viwandani, wilayani Bariadi, Mkoa wa Simiyu.

Uzinduzi huo umefanyika Desemba 15, 2019 ambapo Kituo hicho kinachukua umeme kutoka Kituo Kikuu cha Mabuki kilichopo Wilaya ya Misungwi, mkoani Mwanza umbali wa kilomita 87.2, kupitia Njia ya kusafiri umeme ya Msongo wa kV 33.

Akizungumza na waandishi wa habari kabla ya uzinduzi huo, Dkt Kalemani, alisema kituo hicho kimezinduliwa rasmi kwa lengo la kuimarisha hali ya upatikanaji umeme katika Mkoa wa Simiyu ambao umejikita katika uwekezaji wa Viwanda , na hivyo unahitaji umeme wa uhakika.

Kutokana na uwepo wa Kituo hicho, Dkt. Kalemani alisema "natoa agizo kwa Meneja wa Mkoa, mtafute eneo la kiwanja hapa, mjenge eneo la makazi kwa ajili ya mtumishi atakayekiangalia kituo hiki kwa masaa 24, kwa sababu ikitokea dharura haitowezekana mtu kutembea kilomita 10 kuja hapa hivyo ni lazima mtu akae hapa."

Aidha, Dkt Kalemani alitoa wito kwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, kuwahamasisha wananchi wa eneo hilo kutunza miundombinu ya kituo husika ili wananchi wasifanye uharibu wa aina yoyote katika eneo hilo, ambalo ni muhimu kwenye maendeleo ya shughuli mbali mbali za kiuchumi.

Vile vile, alisema ifikapo mwezi Machi mwakani Kituo Kikuu cha Kupoza umeme cha Imalilo kilichopo wilaya ya Bariadi, mkoani humo nacho kitakuwa kimekamilika ambapo kitawezesha wananchi wa Mkoa huo na maeneo ya jirani kupata umeme wa uhakika na wakutosha kwa ajili ya matumiza ya kawaida na Viwanda vilivyopo mkoani humo.

Aidha, alisema kuwa, Serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 4 kwa Mkoa huo ambazo zinatumika kwa ajili ya kufanya ukarabati wa miundombinu ya umeme iliyoharibika na kusambazia umeme katika maeneo ambayo bado hayajapata umeme.

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka aliishukuru Serikali kwa kazi kubwa inayofanya ili kuhakikisha umeme unapatikana nchi nzima.

Alisema, Mkoa huo unaenda kwenye Mapinduzi ya Viwanda kwa haraka na ujio wa kituo hicho utaharakisha maendeleo ya Viwanda mkoani humo.

Aliongeza kuwa, wawekezaji waliofika mkoani Simiyu walitaka wajenge viwanda karibu na eneo ambalo lipo karibu na kituo hicho cha umeme na Serikali imeridhia ombi hilo.

Katika ziara yake mkoani humo, Waziri wa Nishati, alitembelea eneo kutakapojengwa Kituo cha Kupoza Umeme, Imalilo wilayani Bariadi na kuwasha umeme katika kijiji cha Nyasosi kilichopo wilayani humo.



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ( mwenye shati la bluu) akisalimiana na watumishi mbalimbali wa Mkoa wa Simiyu mara baada ya kufika katika uzinduzi wa Kituo cha Kupokea na Kutawanya Njia kuu za Umeme kilichopo eneo la Ng'ami wilayani Bariadi mkoani humo.*



*Eneo la Kituo cha Kupokea na Kutawanya Njia kuu za Umeme kilichopo katika eneo la Ng'ami wilayani Bariadi mkoani Simiyu.*



*Msimamizi wa cha Kituo cha Kupokea na Kutawanya Njia kuu za Umeme cha Ng'ami, wilayani Bariadi mkoani Simiyu akitoa maelezo kuhusu kituo hicho kwa Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani pamoja wageni alioambatana nao.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Nyasosi wilayani Bariadi kabla ya kuwasha umeme katika eneo hilo.*

# ACHENI KULALAMIKA, TENGENI FEDHA KULIPIA UMEME – DKT KALEMANI



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani, akitoa maelezo ya matumizi ya kifaa cha Umeme Tayari (UMETA) kwa wananchi wa kijiji cha Liganga wilayani Songea, wakati wa hafla ya kuwasha rasmi umeme kijijini hapo, Desemba 11, 2019. Waziri aliwasha umeme katika Kanisa Katoliki la Bikira Maria Mpalizwa Mbinguni, Parokia ya Liganga ikiwa ni kampeni ya uhamasishaji kuunganisha umeme katika taasisi na miradi mbalimbali ya umma zikiwemo nyumba za ibada.

**VERONICA SIMBA – RUVUMA**

Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani amewataka baadhi ya wakurugenzi na wenyeviti wa halmashauri za wilaya ambao wamekuwa wakilalamika kuwa taasisi za umma katika maeneo yao hazina umeme, waachane na malalamiko, badala yake watenge fedha za kulipia huduma hiyo ili wapatiwe umeme.

Aliyasema hayo kwa nyakati tofauti Desemba 11, 2019 akiwa katika ziara ya kazi wilayani Nyasa na Songea, mkoani Ruvuma.

Dkt Kalemani alieleza kuwa, uzoefu alioupata katika ziara zake sehemu mbalimbali nchini unaonesha kuwa sababu ya taasisi nyingi za umma kutounganishiwa umeme ni viongozi wake kutolipia huduma hiyo.

Alisema, wengi wamekuwa wakilalamika, lakini serikali inapofuatilia inagundua kuwa taasisi husika hazijalipia huduma hiyo.

"Wengi wao wanatenga fedha za ujenzi wa taasisi lakini wanasahau kutenga bajeti ya umeme halafu wanalalamika."

Akitoa hamasa zaidi kwa viongozi hao kutekeleza maelekezo yake, Dkt Kalemani aliwataka watumie fursa iliyotolewa na serikali vijijini, ambapo gharama za uunganishaji umeme zimeshushwa.

"Hata taasisi zitakazounganishwa kwa mfumo wa njia tatu (three phase), bado gharama yake ni ndogo sana ukilinganisha na inayotozwa mjini. Badala ya kulipia mamilioni, utalipia laki na sehemu tu hivyo changamkeni."

Katika ziara hiyo, Waziri aliwasha umeme katika vijiji vya Liuli na Kihagala vilivyoko wilayani Nyasa pamoja na vijiji vya Liganga na Nguvumoja vilivyoko wilaya ya Songea.

Aidha, pamoja na mambo mengine, alisisitiza umuhimu wa taasisi za umma na miradi mbalimbali ya maendeleo kupewa kipaumbele katika kuunganisha umeme ili ziweze kuwahudumia vema wananchi.

Waziri aliwapongeza viongozi wa maeneo hayo wakiwemo wabunge Stella Manyanya (Nyasa) na Jenista Mhagama (Peramiho) pamoja na Wakuu wa Wilaya husika, Madiwani na wengine ngazi ya halmashauri na vijiji, kwa kufuatilia utekelezaji wa miradi ya umeme bila kuchoka ili kuhakikisha wananchi wao wanafikiwa na nishati hiyo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya viongozi hao, akiwemo Mbunge wa Nyasa Mhandisi Manyanya pamoja na Mkuu wa Wilaya hiyo, Isabela Chilumba, wameipongeza Serikali kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya umeme inayolenga kuboresha maisha ya wananchi, hususan walioko vijijini.



Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Isabela Chilumba (kushoto), akimweleza Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kulia) na Ujumbe wake, hali ya upatikanaji umeme wilayani humo, wakati wa ziara yake kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme na kuzungumza na wananchi, Desemba 11, 2019.



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (kushoto) akiwa amefuatana na mwenyeji wake, Mbunge wa Nyasa, Mhandisi Stella Manyanya, baada ya kuwasha rasmi umeme katika jengo la Kituo cha Afya cha Kihagala wilayani Nyasa, Mkoa wa Ruvuma, Desemba 11, 2019.



Mbunge wa Nyasa, Mhandisi Stella Manyanya akizungumza na wananchi (hawapo pichani) wakati Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (wa kwanza-kushoto) alipofika kijiji cha Kihagala wilayani Nyasa, kuwasha rasmi umeme, Desemba 11, 2019.

# MATUKIO PICHANI





*Zoezi la kuunganisha umeme likiendelea katika kijiji cha Kihagala wilayani Nyasa, Mkoa wa Ruvuma. Taswira hii ilinaswa Desemba 11, 2019 wakati Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), alipofika kijijini hapo kuwasha rasmi umeme.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (mwenye kipaza sauti) akizungumza na wananchi wa kijiji cha Liuli wilayani Nyasa, mkoani Ruvuma, alipofika kuwawashia rasmi umeme, Desemba 11, 2019*



*Sehemu ya majengo ya Kituo cha Afya cha Kihagala wilayani Nyasa. Hospitali hii iliwashiwa rasmi umeme na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), Desemba 11, 2019.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (wa pili-kushoto), akikata utepe kabla ya kuwasha rasmi umeme katika Kanisa la Bikira Maria Mpalizwa Mbinguni, Parokia ya Liganga, wilayani Songea, Desemba 11, 2019.*

# Mgalu : REA III Mzunguko wa Pili isiache Kijiji



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akizungumza na wakazi wa Kijijizi cha Migude, Kata ya Kiromo, wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, alipofika kuwasha umeme katika kijiji hicho.*



*Mbunge wa Bagamoyo. Dkt. Shukuru Kawambwa akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Migude, Kata ya Kiromo wilayani Bagamoyo mkoani Pwani.*

**NA ZUENA MSUYA, PWANI**

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu amelitaka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuhakikisha kuwa hawaruki kijiji katika mradi wa usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu mzunguko wa Pili unaotarajiwa kuanza mapema mwezi Januari 2020 kwa kuwa awamu hiyo ni ya mwisho katika kuunganisha Vijijini.

Mgalu alisema hayo, Desemba 8, 2019 wakati akiwasha umeme katika Kijiji cha Migude, Kata ya Kiromo wilayani Bagamoyo mkoani Pwani.

Mgalu alifafanua kuwa utekelezaji wa mradi wa REA Awamu ya Tatu mzunguko wa Pili ni wa mwisho katika kusambaza umeme vijijini, miradi itakayofuata ni kusambaza umeme katika Vitongoji, hivyo REA na TANESCO wahakikishe wanashirikisha Serikali za Mitaa ili kuorodhesha vijiji vyote kwa umakini na usahihi ili viweze kupatiwa umeme ifikapo Mwezi, Juni 2021.

Alieleza kuwa, huenda Tanzania inaongoza kwa kuwa ya nchi ya kwanza kwa nchi za Afrika Mashariki katika kusambaza umeme vijijini, ambapo mpaka sasa ina vijiji 8115 vilivyounganishwa na umeme zaidi ya vijiji 12,000 na kwa vijiji zaidi ya 4000 vilivyosalia, kazi ya kusambaza umeme inaendelea.

"TANESCO na REA, hakikisheni hamuachi kijiji, hii ni awamu ya mwisho kwa mradi wa REA mzunguko wa Tatu, "Hii ndiyo Baba lao", hatutarudi nyuma tena kuunganisha umeme vijijini, miradi itakayokuja sasa itakuwa ni maalum kwa ajili ya vitongoji, hivyo basi mshirikishe Serikali za mitaa kuhakikisha hakuna kinachoachwa nyuma na bei ya kuunganishiwa umeme ni shilingi 27,000, pia ni marufuku kuwauzia wateja Nguzo wala LUKU." alisisitiza Mgalu.

Aidha aliipongeza Bodi ya Wakurugenzi ya REA, kwa kukubali na kuridhia maombi ya nyongeza ya Kaya 5000, ambazo ziliomba kuunganishiwa umeme na zoezi hilo likafanyika kwa Mkoa wa Pwani, hivyo alitaka utaratibu huo uendelee kwa maeneo mengine nchini kwa kuwa miradi hiyo imetumia gharama kubwa katika kuitekeleza na lengo ni kuwafikia wananchi wote.

Sambasamba na hilo aliitaka TANESCO kuangalia namna bora na nzuri ya kuwawezesha wateja kulipia gharama za kuunganisha umeme katika majumba yao, ikiwezekana kuwakopesha na baadaye walipie kupitia LUKU au Ankara zao au kuwawekea utaratibu wa kulipia kidogo kidogo ili kila mmoja aweze kuunganishwa na umeme.

Aliwaeleza kuwa TANESCO wasikatae fedha pale mteja anapotaka kulipa kwa awamu, isipokuwa waweke utaratibu mzuri wa malipo hayo kwa lengo la kumsadia mteja yule ambaye hawezi kuzilipa zote kwa mara moja ili aunganishiwe umeme.

Alirudia kusema utaratibu wa bei ya shilingi elfu 27,000 uliotolewa na Serikali kwa miradi ya TANESCO inalenga wateja walio vijijini ambapo kuna miradi ya REA, lakini agizo hilo haliwahusu wateja waliopo kwenye Manispaa na Majiji katika miradi ya TANESCO inayoendela kutekelezwa kwa sababu TANESCO inatakiwa ijiendesha kutokana na mapato yake.

Hata hivyo alisema kuwa kwa sasa Serikali inapokea maoni yanayotaka gharama ya shilingi 27,000 iwe nchi nzima, maoni hayo yatafanyiwa utafiti kwa kina na kuona namna bora ya kupunguza bei ya kuwaunganishia umeme wateja waliopo katika Manispaa na Miji ili kila mmoja aweze kupata huduma hiyo kwa gharama anayoweza kuimudu.



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu,(kushoto) akimtwika ndoo ya maji mmoja wa akina Mama wa Kijiji cha Migude, Kata ya Kiromo, wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, kutoka katika kisima cha maji kinachotumia umeme wa REA baada ya Naibu Waziri kuwasha umeme katika kijiji hicho.*

# WAZIRI KALEMANI AKAGUA UJENZI WA KITUO CHA KUPOZA UMEME BULYANHULU NA KUTOA MAELEKEZO





*Ujenzi kwa ajili ya upanuzi wa kituo cha kupoza umeme Bunyanhulu, wilayani Kahama, Mkoa wa Shinyanga ukiendelea. Taswira hii ilichukuliwa Desemba 4, 2019 wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), kituoni hapo.*

***VERONICA SIMBA – KAHAMA***

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, Desemba 4, 2019 amekagua maendeleo ya ujenzi unaolenga kupanua kituo cha kupoza umeme Bulyanhulu, wilayani Kahama, Mkoa wa Shinyanga na kutoa maelekezo kadhaa kwa uongozi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na mkandarasi husika.

Akiwa amefuatana na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, viongozi mbalimbali wa serikali, vyama vya siasa pamoja na wataalam kutoka wizarani, TANESCO na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Waziri alimwagiza Mkandarasi kukamilisha ujenzi husika ifikapo Mei, 2020.

Alisisitiza kauli hiyo na kusema kuwa muda hautaongezwa hata siku moja, hivyo akamtaka Meneja wa TANESCO mkoani humo kumsimamia mkandarasi ili akamilishe kazi kwa wakati na viwango stahiki.

"Hii ni kazi muhimu sana hivyo lazima ikamilike kwa wakati."Tunapanua kituo hiki ili kukiongezea uwezo kutoka megawati 16 za sasa hadi kufikia megawati 51. Ujenzi ni mkubwa maana utahusisha pamoja na mambo mengine, kujenga njia ya kusafirisha umeme umbali wa kilomita 57 kutoka Bulyanhulu hadi Geita."

Aidha, alieleza kuwa, ujenzi utakapokamilika, kituo hicho kitasaidia kufua na kupitisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 unaotoka Shinyanga kwenda hadi Geita ambako pia kunajengwa kituo kingine kikubwa cha megawati 100.

Akifafanua zaidi, Waziri alisema ujenzi wa kituo cha Geita pamoja na upanuzi wa kituo cha Bulyanhulu, gharama yake ni takribani dola za kimarekani milioni 23 na kwamba mradi unahusisha pia kupeleka umeme kwenye vijiji 10 kutoka Bulyanhulu kupitia Busanda hadi Buseresere.

Katika hatua nyingine, Waziri aliuagiza uongozi wa TANESCO wilayani humo, kuhakikisha vifaa mbalimbali vinavyotumika kuendeshea mitambo katika kituo hicho cha kupoza umeme cha Bulyanhulu, vikiwemo vikata umeme maarufu kama 'circuit breaker' vinabadilishwa mara kwa mara badala ya kusubiri hadi viharibike, suala ambalo limekuwa likisababisha kukatika kwa umeme.

Vilevile, aliagiza ujenzi wa ofisi na nyumba ya kuishi wahudumu wa kituo hicho, uanze mara moja ili kuwawezesha watumishi hao kuishi karibu na kituo, waweze kutoa huduma mara moja pindi linapotokea tatizo kwenye mitambo.

Awali, Waziri alitembelea kijiji cha Igunda wilayani humo, ambapo aliwasha rasmi umeme, Pia, alitembelea kijiji cha Ntobo, Kata ya Msalala na kuwaeleza wananchi kuwa umeme utafikishwa katika kijiji hicho hivi karibuni.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akiwahamasisha wananchi wa kijiji cha Igunda, wilayani Kahama, Mkoa wa Shinyanga (hawapo pichani), kuiga mfano wa bibi Teresia Shotoo (kulia kwa Waziri), aliyelipia shilingi 27,000 na kuunganishiwa umeme kwenye nyumba yake. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi wilayani humo, Desemba 4, 2019.*

# MATUKIO PICHANI



Moja ya kisima cha maji kilichounganishwa na umeme wa mradi wa REA katika Kijiji cha Migude, Kata ya Kiromo, wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu aliwasha umeme katika kijiji hicho.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu( pili kushoto) akikata utepe kuashiria kuwasha umeme katika Kijiji cha Migude, Kata ya Kiromo, wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, alipofika kuwasha umeme katika kijiji hicho.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (pili kushoto) akitoa zawadi ya mifuko ya saruji kwa viongozi wa Serikali za mitaa kusaidia ujenzi wa shule ya msingi katika kijiji hicho kama sehemu ya kusherehekea miaka 58 ya Uhuru wa Tanganyika na miaka 57 ya Jamhuri.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha (kushoto), akimweleza Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kulia), hali ya upatikanaji umeme wilayani humo. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi wilayani Kahama, Desemba 4, 2019.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani) na Ujumbe wake, wakikagua maendeleo ya ujenzi unaohusisha upanuzi wa kituo cha kupoza umeme Bulyanhulu, Desemba 4, 2019.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Mchangani, katika Kisiwa Kome,wilayani Sengerema mkoani Mwanza alipotembelea kijiji hicho wakati wa kukagua usambazaji wa umeme vijijini.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu( katikati) akipita katika mitaa ya nyumba za wakazi wa Kijiji cha Mchangani, kisiwani Kome, wilayani Sengerema mkoani Mwanza alipotembelea kijiji hicho wakati wa kukagua usambazaji wa umeme vijijini.

# Uunganishaji umeme Vijijini uende sambamba na idadi kubwa ya kuwawashia wateja

NA ZUENA MSUYA, MWANZA

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, amewaagiza Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA) pamoja na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuwa kasi ya kuunganisha umeme vijijini iende sambamba na kasi ya kuwawashia Umeme wateja katika Nyumba zao.

Mgalu alisema hayo kwa nyakati tofauti alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme katika Kijiji cha Buchosa na Mchangani Kisiwani Kome wilayani Sengerema, pia katika Kijiji cha Buganda na Dutongo wilayani Ilemela mkoani Mwanza, Desemba 21 na 22, 2019.

Akiwa katika Wilaya hizo, Mgalu alisema kuwa hafurahishwi kuona kasi ndogo ya kuwaunganishia umeme wateja katika vijiji mbalimbali ambavyo tayari vimeunganishwa na umeme, huku kukiwa na wateja wengi wanaohitaji huduma hiyo na tayari wameshalipia.

Aidha aliwataka wakandarasi pamoja na TANESCO kuhakikisha kuwa ndani ya siku saba wawe wamewaunganisha wateja waliolipia umeme, badala ya kuwaacha wateja hao wakisubiri muda mrefu pasipo sababu ya msingi.

"Kwakweli haipendezi kuona vijiji vimeunganishwa na umeme, wanaohitaji ni wengi lakini waliowashiwa ni wachache mno, watu wametandaza nyaya katika nyumba zao, na wamelipia lakini hawajawashiwa umeme,bila sababu ya msingi." alisema Mgalu.

Vilevile, aliwataka TANESCO kutoa taarifa sahihi na kwa wakati kwa wananchi endapo kuna changamoto yoyote inayosababisha mradi kuchelewa ama mtu kutounganishwa kwa wakati na huduma ya umeme ili kuwaondelea hofu wananchi hao na kuwajengea uwezo wa uelewa zaidi namna ambavyo mradi huo unatekelezwa katika maeneo yao.

Akiwa, katika Wilaya ya Sengerema, Mgalu aliwasha umeme katika Kijiji cha Buchosa na kutembelea Kijiji cha Mchangani kilichopo katika hifadhi ya Kisiwa cha Kome na kuzungumza na wananchi.

Baada ya kusikiliza malalamiko ya wananchi na kuridhishwa na mazingira ya eneo husika, aliahidi kuwapatia umeme wananchi hao waliokuwa wakiusubiri kwa muda mrefu baada ya kufanya mazungumzo na Wizara ya Maliasili na Utalii ili kuona namna bora ya kufikisha huduma hiyo eneo hilo.

Wakazi wa eneo hilo awali walitakiwa kupisha eneo la hifadhi katika Kijiji hicho na hawakuwa wakipatiwa huduma muhimu ikiwemo umeme kwa kile kinachoelezwa kuwa wamevamia eneo la hifadhi, na kufanya shughuli za uvuvi na biashara mbalimbali.

Hata hivyo, uongozi wa Kijiji ulimueleza Mgalu kuwa, Wizara yenye dhamana ya kusimamia hifadhi hiyo imetoa kibali cha kuwaruhusu wananchi hao kuendelea kuishi eneo hilo kwa sharti la kutojenga nyumba za kudumu, kulinda na kutunza hifadhi hiyo wakati wakiendelea na shughuli zao.

Katika Wilaya ya Ilemela, Mgalu aliwasha umeme katika Kijiji Buganda na Dutongo, ambapo pamoja na mambo mengine aliwataka wananchi kuendelea kulipia gharama za kuunganishiwa umeme ya shilingi 27,000 tu, pia wasikubali kutozwa gharama za nguzo, nyaya wala mita kwakuwa gharama hizo zimegharamiwa na Serikali.

Pia aliwaeleza kuwa hakuna kiijiji wala kaya itakayorukwa wala kuachwa kuunganishiwa umeme, hivyo wawe na subira kwa kuwa watapatiwa umeme.





Muonekano wa nyumba za Kijiji cha Mchangani katika hifadhi ya Kisiwa cha Kome, wilayani Sengerema mkoani Mwanza, zinazohitaji kuwekewa umeme.

# MATUKIO *PICHANI*




*Wakazi wa Kijiji cha Mchangani katika Kisiwa cha Kome wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu,( hayupo pichani) kuhusu ombi lao la kupatiwa umeme katika makazi yao.*



*Mbunge wa Jimbo la Buchosa, Charles Tizeba akizungumza na wakazi wa eneo hilo, wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu wilayani Sengerema mkoani Mwanza wakati wa kukagua usambazaji wa umeme vijijini.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Buganda,wilayani Ilemela mkoani Mwanza wakati wa kukagua usambazaji wa umeme vijijini.*



*Naibu waziri wa Nishati, Subira Mgalu( kushoto) akiteta jambo na Kaimu Meneja wa TANESCO mkoani Mwanza katika kijiji cha Buganda, wilayani Ilemela mkoani Mwanza wakati wa kukagua usambazaji wa umeme vijijini.*





*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akikata utepe kuashiria kuwasha umeme katika Kijiji cha Buganda, wilayani Ilemela mkoani Mwanza wakati wa kukagua usambazaji wa umeme vijijini.*

*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akiwasha umeme katika shule ya kijiji cha Dutongo, wilayani Ilemela mkoani Mwanza wakati wa kukagua kazi ya usambazaji wa umeme vijijini.*

# WASIOUNGANISHA UMEME KUCHUKULIWA HATUA



*Waziri wa Nishati, Dkt, Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa kijiji cha Chemkeni wilayani Kaliua, Mkoa wa Tabora mara baada ya kuwasha umeme kijijini humo.*

***HAFSA OMAR- TABORA***

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amesema Serikali itaanza kuchua hatua kwa wananchi wote ambao hawataunganisha umeme kwenye nyumba zao, ambao wana uwezo wa kulipia shilingi 27,000.

Aliyasema hayo, Desemba 22, 2019 katika kijiji cha Chemkeni kilichopo, kata ya Igwisi, Wilaya ya Kaliua, Mkoani Tabora, wakati alipokuwa akifanya ukaguzi wa nyumba ambazo hazijaunganishwa umeme kijijini humo.

Alieleza kuwa, Serikali inatumia gharama kubwa kuhakikisha umeme unafika nchi nzima, kwahiyo asingependa kuona wananchi hawatumii fursa hiyo kuweka umeme kwenye nyumba zao tena kwa gharama nafuu.

Aidha, Dkt. Kalemani alisikitishwa na kitendo cha baadhi ya wakazi wa kijiji hicho, kukataa kuweka umeme kwenye nyumba zao kwa madai ya kwamba wanasubiri kufungua biashara ambazo zitawalazimu kuunganisha umeme.

"Haiwezekani Serikali ilete bilioni 36 kwenye Mkoa huu, halafu mkatae kutumia umeme, nitarudi hapa mwakani kufuatilia nyumba kwa nyumba." alisema.

Vilevile, Waziri Kalemani, aliwaagiza TANESCO kuendelea kuwahamasisha wananchi kulipia huduma ya umeme ili wananchi wapate hamasa ya kuweka umeme kwenye nyumba na taasisi za umma ambazo zipo karibu na maeneo yao.

Katika ziara yake mkoani humo, Waziri wa Nishati, aliambatana na Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Abel Busalama, Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga na viongozi mbalimbali wa vyama na Serikali.

Pia aliwasha umeme katika vijiji vya Ilege, Chemkeni vilivyopo wilayani Kaliua na kukagua ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Uhuru kilichopo wilaya ya Urambo.



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani( mwenye shati la bluu) pamoja na viongozi mbalimbali wakielekea kuwasha umeme kwenye shule iliyopo kwenye kijiji cha Chemkeni wilayani Kaliua, Mkoa wa Tabora.*



*Wananchi wa kijiji cha Chemkeni wilayani Kaliua, Mkoa wa Tabora wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt, Medard Kalemani alipokuwa akiwahutubia kijijini humo.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akikata utepe kuashiria kuwasha kwa umeme katika kijiji cha Chemkeni wilayani Kaliua, Mkoa wa Tabora.*

# UMEME UMEBADILI MAISHA YA WANA-RUVUMA – RC MNDEME

**VERONICA SIMBA – RUVUMA**

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme ameipongeza Serikali kwa kuunganisha umeme wa gridi ya Taifa mkoani humo, ambao umebadili hali ya maisha ya wananchi husika kutoka kwenye uduni na kuwa bora zaidi.

Alikuwa akieleza hali ya upatikanaji umeme mkoani Ruvuma kwa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na Ujumbe wake, ambaye alimtembelea ofisini kwake akiwa katika ziara ya kazi, Desemba 12, 2019.

"Tunamshukuru sana Rais John Pombe Magufuli kwa kutuletea umeme. Sisi tangu nchi inapata Uhuru, tulikuwa hatujawahi kupata umeme wa gridi; Sasa hivi tunafurahia umeme kila uchao."

Akifafanua mabadiliko chanya yaliyoletwa na umeme kwa wananchi wa Ruvuma, Mkuu huyo wa Mkoa alisema yamejikita hasa katika shughuli za kimaendeleo.

Alisema, mashine za kusaga mahindi zilizokuwa zinatumia mafuta ya dizeli na ambazo zilikuwa nyingi, kwa kiasi kikubwa hazipo tena badala yake mashine nyingi sasa zinatumia umeme.

Alieleza zaidi kuwa, uwepo wa mashine zinazotumia umeme kusaga nafaka, kumepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za kusaga nafaka hizo kwa wananchi ambao hutumia unga wa mahindi kupikia ugali, ambacho ni chakula chao kikuu.

Vilevile, alieleza kuwa vijiji vingi sasa vimekuwa na mwanga wa umeme hasa nyakati za usiku, tofauti na ilivyokuwa awali, ambapo vijijini kulikuwa na giza totoro.

Kufuatia suala hilo, aliipongeza serikali kwa kupitisha na kutekeleza azimio la kutobagua aina ya nyumba wakati wa kuunganisha umeme na kusema kuwa wananchi wengi wa maisha ya chini wanafurahia umeme kama wengine wenye kipato cha juu pasipo kujiona wametengwa.

Aidha, alishukuru kwa kazi inayoendelea ya kujenga miundombinu ya umeme ili kupeleka gridi ya Taifa wilayani Tunduru huku akibainisha kuwa ndiyo wilaya pekee mkoani humo ambayo haijafikiwa na umeme wa gridi ya Taifa.

Kwa upande wake, Waziri wa Nishati alimweleza Mkuu huyo wa Mkoa kwamba kazi ya ujenzi wa miundombinu ya kupeleka umeme wa gridi Tunduru imekamilika na kwamba katika ziara yake amejiridhisha na hilo.

"Wataalamu wamefanya kazi nzuri sana na kwa sasa wanakamilisha kazi ndogo ndogo tu. Tunatarajia siku yoyote kuanzia hivi sasa, tutazima mitambo ya mafuta Tunduru na kuunganisha umeme wa gridi ya Taifa."

Katika hatua nyingine, Waziri aliahidi kuwashawishi wawekezaji waende mkoani humo kufanya tathmini kwa ajili ya kuanzisha kiwanda cha kutengeneza nguzo.

Alitoa ahadi hiyo kufuatia maombi ya Mkuu wa Mkoa ambaye alimweleza kuwa mkoa huo pia umejaaliwa kuwa na miti mingi hivyo ingefaa kukawa na kiwanda hicho ili kuunga mkono juhudi za serikali kutumia vifaa vya kuunganishia umeme ambavyo vinatengenezwa ndani ya nchi.



*Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme (kushoto), akizungumza na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, kuhusu hali ya upatikanaji umeme mkoani humo. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi, Desemba 12, 2019.*



*Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme (Meza Kuu-katikati), akizungumza na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na Ujumbe wake, kuhusu hali ya upatikanaji umeme mkoani humo. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi, Desemba 12, 2019.*

## MATUKIO *PICHANI*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa Ilege wilayani Kaliua mkoa wa Tabora kabla ya kuwasha umeme kijijini humo.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani na viongozi mbalimbali wa Wilaya ya Kaliua na Wizara ya Nishati wakiwa katika kituo cha kupoza umeme cha Uhuru kilichopo wilayani Urambo, Mkoa wa Tabora ambacho ujenzi wake unaendelea.*

# DKT. KALEMANI AAGIZA WAKANDARASI WA UMEME KIGOMA KUWEKWA NDANI



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Nguruka wilayani Uvinza, Mkoa wa Kigoma katika mkutano wa hadhara uliofanyika kijiji humo.*



*Wananchi wa Kijiji cha Nguruka wilayani Uvinza, Mkoa wa Kigoma wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani wakati akihutubia kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kijijini humo.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akitoa maelekezo kwa wakandarasi wa kampuni ya ETERN-CCCE ambao wameonesha kusuasua katika kazi ya usambazaji umeme mkoani Kigoma.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (katikati) akitoa maagizo kwa Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Mwanamvua Mrindoko ( kushoto) ya kuwachukulia hatua wakandarasi wa kampuni ya ETERN-CCCE baada ya kutoridhishwa na kazi yao ya kusambaza umeme vijijini mkoani Kigoma.*

***HAFSA OMAR-KIGOMA***

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ametoa agizo kwa Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Mwanamvua Mrindoko kuwaweka ndani na kuwanyang'anya hati za kusafiria, wakandarasi wa kampuni ya ETERN-CCCE waliopewa kazi ya kusambaza umeme vijijini mkoani Kigoma baada ya kusuasua katika utekelezaji wa kazi.

Alitoa agizo hilo Desemba 22, 2019, akiwa katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji cha Nguruka, Wilaya ya Uvinza, Mkoani Kigoma, katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme mkoani humo.

Alisema amechukua hatua hiyo mara baada ya kukagua kazi ya usambazaji umeme mkoani humo na kuona maeneo mengi yakiwa bado hayajasambaziwa umeme kutokana na kusuasua katika kazi kwa mkandarasi huyo.

" Wameanza kazi lakini spidi yao ni ya kusuasua sana, spidi yao hairidhishi huo ndio ukweli, lakini hatuwezi kubaki tunalalamika lazima tuanze kuchukua hatua, leo nimekuja kukagua hapa nimekuta amewasha vijiji Saba tu ambapo zaidi ya vijiji hamsini bado havijawashwa." Alisema

Dkt. Kalemani, pia alichukizwa na kitendo cha wakandarasi hao kufanya kazi kwa udanganyifu kwa kuweka nguzo na transfoma katika eneo hilo siku moja kabla ya ziara yake kijijini humo, na kuwataka wakandarasi hao kufanya kwa mujibu wa mkataba.

Vile vile, aliwaagiza wakandarasi hao kuwa, ifikapo Januari 10 mwakani wawe tayari wamewasha umeme katika kijiji hicho na Vitongoji vyake vyote na kuongeza spidi ya kufanya kazi pamoja kuajiri vibarua wengi ili kasi ya usambazaji umeme iongezeke.

Katika ziara yake mkoani humo, Waziri wa Nishati, alikagua ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nguruka, kituo ambacho kikikamilika Mkoa wa Kigoma utaunganishwa na gridi ya taifa.

# WANANCHI VIJIJINI SASA KULIPIA UMEME KWA KUDUNDULIZA



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akiwasha rasmi umeme katika kijiji cha Mnekezi, wilayani Chato, Mkoa wa Geita, akiwa katika ziara ya kazi, Desemba 3, 2019.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati-mwenye kipaza sauti), akizungumza na wananchi wa kijiji cha Mnekezi, wilayani Chato, Mkoa wa Geita, kabla ya kuwasha rasmi umeme kijijini hapo, Desemba 3, 2019. Kulia kwake ni Mkuu wa Wilaya ya Chato, Charles Kabeho.*

VERONICA SIMBA – CHATO

Wananchi wa maeneo ya vijijini ambao hawana uwezo wa kulipia shilingi elfu 27 za kuunganishiwa umeme kwa mkupuo, sasa wanaweza kulipia huduma hiyo kwa kudunduliza kidogo kidogo.

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani aliyasema hayo Disemba 3, 2019 kijijini Mnekezi, wilayani Chato, ambapo alikuwa akizungumza na wananchi kabla ya kuwasha rasmi umeme kijijini hapo.

Alikuwa akitoa maelekezo kwa wataalamu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwamba, wahakikishe wananchi wote wanaunganishiwa umeme bila kubagua hali zao kiuchumi kama ilivyo azma ya serikali.

Alisema kuwa, pamoja na Serikali kupunguza gharama za kuunganisha umeme vijijini hadi shilingi elfu 27 tu lakini bado wako wananchi ambao kipato chao hakiwezi kuwaruhusu kulipa pesa hiyo kwa mkupuo, hivyo akawataka watendaji hao kupokea malipo ya wananchi husika kwa mtindo wa kudunduliza.

"Akipata elfu 10 akaleta, pokea umwandike; kesho akileta nyingine elfu tano pokea hadi pale atakapotimiza kiwango kinachotakiwa cha elfu 27."

Katika hatua nyingine, Waziri alitoa hamasa kwa wananchi wa kijiji hicho na vingine vyote nchini ambako miradi mbalimbali ya umeme inatekelezwa, kutochagua kazi.

Alitoa hamasa hiyo baada ya kutoa maagizo kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini nchi nzima, kuhakikisha wanaajiri vibarua kutoka maeneo husika ili kuharakisha kazi lakini pia kuinua kipato cha wananchi, hususan vijana wa maeneo hayo.

Aidha, aliwataka wananchi kuachana na kasumba ya kulalamika kuwa hawajaunganishiwa umeme wakati hawajalipia huduma husika kwa visingizio tofauti, ikiwemo madai ya ukosefu wa nguzo.

"Wananchi, suala hili narudia tena kulisemea; ninyi mnachotakiwa kufanya ili muunganishiwe umeme ni kulipia tu na kuandaa nyumba zenu kwa kuweka mfumo wa nyaya. Suala la nguzo na vifaa vingine haliwahusu. Lipieni ili mletewe umeme," alisisitiza.

Waziri Kalemani, ambaye pia ni Mbunge wa eneo husika (Chato), aligawa kwa wananchi wa Mnekezi, vifaa 50 vya Umeme Tayari (UMETA) bure, mbali na vile 250 ambavyo kila mkandarasi wa miradi ya umeme vijijini hutakiwa kugawa katika eneo lake la kazi.

Katika ziara hiyo, Waziri alifuatana na viongozi mbalimbali, akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Chato, Charles Kabeho.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (mwenye miwani), akifuatana na Mkuu wa Wilaya ya Chato, Charles Kabeho (wa tatu-kulia), kwenda kuwasha umeme katika moja ya nyumba za wananchi wa kijiji cha Mnekezi, wilayani Chato, Mkoa wa Geita, Desemba 3, 2019.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akitoa maelekezo kwa wafanyakazi wa mkandarasi wa umeme vijijini, anayetekeleza mradi huo katika kijiji cha Mnekezi, wilayani Chato, Mkoa wa Geita, akiwa katika ziara ya kazi, Desemba 3, 2019. Waziri aliwasha rasmi umeme katika kijiji hicho.*



Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani, akitunza moja ya kikundi cha waimbaji cha kijiji cha Kakeneno kabla ya kuwasha umeme katika kijiji hicho.



Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kakeneno ambao walijitokeza kwa wingi kumsikiliza kiongozi huyo.

# UMEME NI USALAMA WEKENI KWENYE NYUMBA ZENU- WAZIRI KALEMANI

HAFSA OMAR- GEITA

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, amesema kuweka umeme kwenye nyumba ni kujihakikishia usalama ndani ya nyumba na inasaidia kuepuka madhara mbalimbali yatokanayo na binadamu, wadudu na wanyama wakali.

Ameyasema hayo, Desemba 17, 2019 katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji cha Kakeneno, kata ya Nyarutembo, Wilaya ya Chato, mkoani Geita kabla ya kukiwashia umeme kijiji hicho.

"Nyumba inapokuwa giza kuna hatari wa wanyama wakali au wadudu wenye sumu kuingia bila ya wewe kuwaona, anaweza kuingia Nyoka, Nge na kusababisha madhara makubwa, lakini nyumba ikiwa na umeme utawaona na utaweza kukabiliana nao." Alisema

Vilevile, aliwahimiza wananchi kujenga viwanda vidogo vidogo ambavyo vitawasaidia kujikwamua kiuchumi na kuviunganisha na umeme, kwa sababu utumiaji wa umeme kwenye viwanda hivyo utawasaidia kupata faida nyingi kulinganisha na utumiaji wa mafuta.

" Nimefurahi kuona mashine ya kukoboa na kusaga mahindi hapa, unganisheni mashine hizo na umeme, ukiwa na umeme badala ya kupata mabede manne kwa siku utapata madebe kumi kwa siku." Aliongeza

Naye, Katibu Kata, Emmanuel Ruzigamazi alisema ujio wa umeme katika kijiji hicho utaleta mabadiliko mengi ya kiuchumi kwani wananchi wa kijiji hicho walikuwa wanausubiri umeme kwa muda mrefu ili kuutumia kwa shughuli mbalimbali ikiwemo za kiuchumi.

Pia aliipongeza Serikali kwa kupeleka umeme katika kijiji hicho, ambacho kabla ya kuwepo kwa umeme kulikuwa na changamoto kubwa kwenye zahanati ambapo baadhi ya wagonjwa walikosa huduma kwa sababu ya kukosekana kwa nishati hiyo, ila kwa sasa huduma zitazidi kuboreka.



Wananchi wa kijiji cha Kakeneno, kata ya Nyarutembo wilayani Chato wakimsikiliza Waziri wa Nishati,Dkt Medard Kalemani , (hayupo pichani) wakati alipofika kijijini hapo kuwasha umeme.




Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akikata utepe kuashiria kuwashwa kwa umeme katika kijiji cha Kakeneno kata ya Nyarutembo wilayani Chato Mkoa wa Geita.

# MATUKIO *PICHANI*

*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani,( mwenye shati la bluu) akiagana na wananchi wa kijiji cha Kakeneno mara baada ya kuwasha umeme katika kijiji hicho.*



*Katibu kata wa kijiji cha Kakeneno Emmanuel Ruzigamazi akizungumza kwenye mkutano wa hadhara kabla ya Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani hajawasha umeme katika kijiji hicho.*





*Wafanyakazi wa kampuni ya mkandarasi wa umeme vijijini ambaye anatekeleza mradi huo katika kijiji cha Mnekezi, wilayani Chato, wakiendelea na kazi husika, baada ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), kukagua kazi hiyo na baadaye kuwasha rasmi umeme katika kijiji hicho.*




*Msikiti uliopo katika kijiji cha Mnekezi, wilayani Chato, Mkoa wa Geita. Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), Desemba 3, 2019, akiwa kijijini hapo, alisisitiza taasisi za umma, nyumba za ibada kama hiyo na miradi ya wananchi ipewe kipaumbele katika kuunganisha umeme.*

# DKT KALEMANI AITAKA TANESCO KUBAINI VYANZO VIPYA YA UMEME

Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani ameiagiza Bodi na Menejimenti ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuhakikisha kuwa wanafanya tafiti kubaini vyanzo vipya vya uzalishaji umeme ili kuongeza kiasi cha nishati hiyo nchini na kuweza kufikia lengo la kuwa na megawati 10,000 ifikapo mwaka 2025.

Dkt.Kalemani alitoa agizo hilo tarehe 19 Disemba, 2019 jijini Dar es Salaam wakati wa kikao kati ya Bodi/Menejimenti ya TANESCO na Wizara ya Nishati ambapo kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu na Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga.

"Lazima tufanye tafiti kubaini vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme ukiacha hivi vilivyopo, hata kama tusipotekeleza leo, vizazi vijavyo vitatekeleza miradi hiyo, mfano tafiti za mradi wa umeme wa Julius Nyerere (MW 2115) zilifanyika miaka mingi iliyopita, lakini mradi tunautekeleza sasa, hivyo nasi hatuna budi kuibua vyanzo vingine." Alisema

Aidha, Dkt Kalemani aliiagiza Bodi na Menejimenti ya TANESCO kuhakikisha kuwa maeneo yote nchini yanaunganishwa na umeme wa Gridi ifikapo mwezi Juni 2022 ili wananchi wapate umeme wa uhakika na pia Serikali kuokoa fedha zinazotumika kununulia Mafuta ili kuendesha mitambo ya umeme kwenye baadhi ya maeneo nchini.

Kuhusu kazi ya usambazaji umeme vijijini, alisisitiza kuwa lengo la Serikali ni kufikisha umeme kwenye vijiji vyote ifikapo mwezi Juni mwaka 2021 na asilimia 85 ya wananchi wanapata umeme hivyo TANESCO ina jukumu la kuhakikisha kuwa lengo hilo linafanikiwa.

Vilevile, Dkt Kalemani aliiagiza TANESCO kuhakikisha kuwa, kila kiwanda au Taasisi ya umma inapojengwa, inafikishiwa umeme lengo likiwa ni kuongeza mapato ya Shirika na pia kuboresha upatikanaji wa huduma za kijamii nchini.

Aidha, aliiagiza Bodi na Menejimenti ya TANESCO kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Shirika kutoka shilingi Bilioni 46 zinazokusanywa sasa kwa wiki hadi kufikia Bilioni 52 kwa Wiki.

Dkt. Kalemani aliongeza kuwa, Shirika hilo pia linapaswa kumaliza madeni yake ifikapo mwaka 2026, linaboresha nidhamu ya watumishi ili kuweza kutoa huduma bora kwa wananchi na kuhakikisha kunakuwa na mpango wa ukarabati wa miundombinu ya umeme kwenye maeneo yote nchini.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, pamoja na kuipongeza TANESCO kwa majukumu mbalimbali wanayofanya, aliiagiza Bodi kujielekeza pia kwenye ukusanyaji wa madeni ya TANESCO kutoka kwa wateja mbalimbali zikiwemo Taasisi za umma kwani fedha zitakazopatikana zitasaidia Shirika kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Aidha, aliiagiza TANESCO kuangalia suala la malipo ya huduma ya umeme ili kuwe na utaratibu wa malipo hayo kufanyika kwa awamu ili kuweza kuunganishia umeme wananchi wengi zaidi na hivyo miradi hiyo ya umeme kuleta tija.

Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga, alisema kuwa, hali ya umeme nchini imeimarika hivyo TANESCO inapaswa kujikita pia kwenye kazi ya kuongeza wateja wa nishati hiyo ili kuongeza mapato.

Vilevile, alisisitiza kuhusu suala la mikoa yote nchini kuunganishwa na gridi ya Taifa ili kuimarisha hali ya umeme kwenye mikoa hiyo.



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akiwa kwenye kikao chake na Bodi/Menejimenti ya TANESCO kilichofanyika jijini Dar es Salaam. Kushoto kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu na kulia kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO, Dkt. Alexander Kyaruzi.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (kushoto), Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga (katikati) na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt. Tito Mwinuka wakiwa kwenye kikao cha uongozi wa Wizara ya Nishati na Bodi na Menejimenti ya TANESCO kilichofanyika jijini Dar es Salaam.*



*Baadhi ya Wajumbe wa Bodi ya TANESCO, wakiwa kwenye kikao cha uongozi wa Wizara ya Nishati na Bodi hiyo pamoja na Menejimenti ya TANESCO kilichofanyika jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akiwa kwenye kikao chake na Bodi/Menejimenti ya TANESCO kilichofanyika jijini Dar es Salaam. Kushoto kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu na kulia kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO, Dkt. Alexander Kyaruzi.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu na Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga wakiwa kwenye kikao chao na Bodi na Menejimenti ya TANESCO kilichofanyika jijini Dar es Salaam.*

# Wawekezaji/Wafanyabiasha Dar es Salaam waridhishwa na huduma ya umeme



Naibu waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akizungumza na Wawekezaji na Wafanyabiashara wakati wa Mkutano kati ya Serikali, Wawekezaji na Wafanyabiashara, uliofanyika jijini Dar es Salaam.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, (kushoto) na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega wakiwasikiliza Wawekezaji na Wafanyabiashara wakati wa Mkutano kati ya Serikali, Wawekezaji na Wafanyabiashara, uliofanyika jijini Dar es Salaam.

**NA ZUENA MSUYA**
**DAR ES SALAAM,**

Naibu waziri wa Nishati, Subira Mgalu amesema huduma ya umeme itaendelea kuboreshwa kwa wafanyabiasha na wawekezaji mbalimbali licha ya kuwa hakuna changamoto inayowakabili wadau hao kwa mkoa wa Dar es Salaam.

Mgalu ilimlazimu kueleza hayo baada ya kudhihirika kuwa hakukuwa na changamoto yeyote inayohusu sekta ya nishati iliyoelezwa na Wawekezaji na Wafanyabiasha wakati wa Mkutano kati ya Serikali, Wawekezaji na Wafanyabiashara, uliofanyika jijini Dar es Salaam, Desemba 6, 2019.

Mkutano huo uliwashirikisha Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wakuu wa Taasisi na Mashirika mbalimbali ukiongozwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji, Angela Kairuki kwa lengo la kutoa fursa kwa wawekezaji na wafanyabiashara kueleza changamoto mbalimbali zinazowakabili katika shughuli zao za kila siku ili zipatiwe ufumbuzi.

Katika, Mkutano huo wafanyabiashara na wawekezaji hawakueleza changamoto yeyote inayohusu sekta ya nishati tofauti na walivyokuwa wakieleza changamoto zinazowakabili katika sekta nyingine, hivyo ilidhihirisha wazi kuwa katika sekta ya nishati hakuna changamoto.

" Nilikuwa nawasikiliza kwa makini sana, lakini sikusikia changamoto katika sekta ya nishati, hii ni dhahiri kwamba nishati inajitahidi katika kuhakikisha mnafanya shughuli zenu bila kikwazo chochote, tutaendelea kuboresha na kuimarisha sekta hii kwa kuwa ndiyo muhimili mkuu kwa maendeleo ya nchi na viwanda." alisema Mgalu.

Mpaka sasa tayari mikoa Saba imekwishafanya mikutano kama hiyo ambayo ni agizo la Rais, Mhe. Dkt, John Pombe Magufuli alilolitoa kwa Mawaziri baada ya kufanya kikao na wafanyabiashara hao mwanzoni mwa mwezi Juni mwaka, 2019.






Baadhi ya wawekezaji na wafanyabiashara wa mkoa wa Dar es Salaam, wakiwasikiliza Mawaziri, Naibu Mawaziri ( hawapo pichani) wakati wa Mkutano kati ya Serikali, Wawekezaji na Wafanyabiashara, uliofanyika jijini Dar es Salaam



Mawaziri na Naibu Mawaziri walioshiriki katika mkutano baina ya Serikali, Wawekezaji na Wafanyabiashara wakiwa katika picha ya pamoja na sekretarieti iliyofanikisha mkutano huo uliofanyika mkoani Pwani.

# Serikali kupunguza bei ya kuunganisha umeme katika Miji na Manispaa

**NA ZUENA MSUYA, DAR ES SALAAM,**

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu amesema Serikali inaangalia namna ya kufanya tathmini ya kupunguza bei ya kuunganisha umeme kwa wateja waliopo katika Miji na Manispaa ili huduma hiyo iweze kumfikia kila mmoja na kuondoa malalamiko.

Mgalu alisema hayo, Desemba 6, 2019, baada ya kubaini changamoto mbalimbali zilizoibuliwa na wawekezaji na wafanyabiara katika Mikutano ya Mashauriano baina ya Serikali, Wawekezaji na Wafanyabiashara, iliyofanyika katika Mikoa ya Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.

Alieleza kuwa, changamoto kubwa iliyokuwa ikizungumzwa katika sekta ya nishati katika mikutano hiyo ni pamoja na tofauti ya bei ya kuunganisha umeme kwa wateja waliopo katika Vijiji, Miji na Manispaa, kuwa haziendani na mazingira halisi ya eneo husika.

Mgalu alisema kuwa, wafanyabiashara na wawekezaji wengi wamedai kuwa, pamoja na Serikali kuweka kiwango cha bei ya Shilingi 27,000 kwa kuunganishiwa umeme vijijini lakini wamekuwa wakitozwa kiwango kikubwa cha fedha tofauti na ilivyoelekezwa kwa madai kuwa wapo katika maeneo ambayo hayakupitiwa na mradi wa usambazaji umeme vijijini REA hali yakuwa wapo vijijini.

Hata hivyo, alisema kuwa Serikali inatambua hali hiyo na kwamba inaangalia namna ya kupunguza bei ya kuunganisha umeme hadi maeneo hayo ya majiji na manispaa ili kila mwananchi apate huduma hiyo kwa urahisi na kwa bei nafuu.

Alitumia mkutano huo kuwaelekeza wafanyabiashara na wawekezaji wenye changamoto za umeme kuwa, wafike Wizara ya Nishati ili waweze kutatuliwa changamoto hizo kwa kuwa nishati ya umeme ni moyo wa uchumi na bila umeme hakuna viwanda.

Mikutano hiyo ilihudhuriwa na Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Kiserikali na Binafsi ambapo tayari Mikoa saba imekwishafanya mikutano kama hiyo ambayo ni agizo la Rais, Mhe. Dkt, John Pombe Magufuli alilolitoa kwa Mawaziri baada ya kufanya kikao na wafanyabiashara hao mwanzoni mwa mwezi Juni mwaka 2019.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akizungumza wakati wa mkutano baina ya Serikali, wawekezaji na wafanyabiashara, uliofanyika mkoani Pwani.



Baadhi ya wawekezaji na wafanyabiashara wakiwasikiliza Mawaziri na Naibu Mawaziri wakati wa mkutano baina ya Serikali, Wawekezaji na Wafanyabiashara uliofanyika Dar es salaam.

# AGIZO LA WAZIRI KALEMANI KUPELEKA UMEME KABUKOME LAAMSHA NDEREMO

**VERONICA SIMBA – BIHARAMULO**

Wananchi wa kijiji cha Kabukome, Kata ya Nyalubungo, wilayani Biharamulo, Mkoa wa Kagera, wameruka kwa nderemo na vifijo, wakifurahia maagizo aliyoyatoa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani Desemba 5, 2019, kuwa kijiji hicho kiwe kimewashiwa umeme ifikapo Januari 30 mwakani.

Waziri alitoa maagizo hayo mbele ya umati wa wananchi wa kijiji hicho, kwa watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wakala wa Nishati Vijijini (REA) pamoja na Mkandarasi anayetekeleza miradi ya umeme vijijini wilayani Biharamulo.

"Leo ni tarehe 5 Desemba; Nataka kuona ikifika tarehe 20 mwezi huu, nguzo ziwe zimeshaanza kusimikwa hapa Kabukome, na tarehe 2 Januari, zianze kupelekwa kijiji cha Lusabya," aliagiza Waziri.

Akieleza kuhusu mpango wa upelekaji umeme katika vijiji mbalimbali vya wilaya hiyo, Dkt Kalemani alisema, vijiji hivyo viwili ambavyo ndivyo pekee havijapata umeme kati ya sita vya kata husika; havikuwa kwenye mpango wa awamu ya kwanza ya uunganishaji umeme vijijini na kwamba viko katika awamu ya pili inayotarajiwa kuanza Aprili, 2020.

"Lakini kwa kutambua shauku kubwa ya umeme mliyonayo wananchi wa Kabukome na Lusabya, serikali imeamua kuwawahishia huduma hiyo muhimu, ili nanyi mnufaike kama wananchi wengine walio na umeme."

Vilevile, Waziri aliwataka TANESCO kuanzisha ofisi ndogo eneo hilo mahsusi kwa wananchi kulipia gharama za kuunganishiwa umeme ili kuwaepusha na usumbufu wa kusafiri mwendo mrefu kufuata huduma hiyo.

Aidha, aliwahamasisha wananchi kuanza mara moja maandalizi ya kuunganishiwa umeme kwa kusuka mfumo wa nyaya (wiring) katika makazi yao pamoja na majengo mbalimbali ya taasisi za umma zikiwemo shule, nyumba za ibada na vituo vya afya.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, viongozi mbalimbali wa kijiji hicho, akiwemo mwenyekiti wake, Kisabo Dominic, walipongeza kazi nzuri inayofanywa na serikali ya awamu ya tano, chini ya uongozi wa Rais John Pombe Magufuli, kuhakikisha wananchi wanyonge wanafikiwa na huduma mbalimbali za kimaendeleo hususan nishati ya umeme.

Pia, walimpongeza Waziri Kalemani pamoja na watendaji wengine wote wa wizara kwa uchapakazi wake na ushirikiano ambao wamekuwa wakitoa kwa wananchi.

Takwimu zinaonesha kuwa, hadi sasa vijiji 51 kati ya 74 vya Wilaya ya Biharamulo vimekwishaunganishiwa umeme.



*Viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), ambao waliambatana na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), katika ziara yake kijijini Kabukome, Wilaya ya Biharamulo, mkoani Kagera, Desemba 5, 2019 wakiwa wamesimama mbele ya wananchi kwa ajili ya utambulisho.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani, akikabidhi vifaa vya Umeme Tayari (UMETA) kwa wananchi wa kijiji cha Kabukome, wilayani Biharamulo, Mkoa wa Kagera, alipokuwa katika ziara ya kazi, Desemba 5, 2019.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kabukome, wilayani Biharamulo, Mkoa wa Kagera, akiwa katika ziara ya kazi, Desemba 5, 2019.*